



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE



TAARIFA KWA UMMA

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale inautangazia Umma kuwa imepokea Jumla ya **Tsh. 1,381,480,029** kutoka Serikali Kuu.

Fedha hizo zinahusisha ujenzi wa Miundombinu ya Elimu ya Sekondari kupitia Programu ya **SEQUIP** kwa mwaka 2023/2024.

Kiasi cha **Tsh. 356,000,000** kimepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Kidato cha 5 na 6 Shule ya Sekondari Bukwimba.

Kiasi cha **Tsh. 584,280,029** kimepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa Shule Mpya ya Sekondari Kata ya Kharumwa ili kupunguza Msongamano Shule ya Sekondari Msalala.

Kiasi cha **Tsh. 441,200,000** kimepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Kidato cha 5 na 6 Shule ya Sekondari Busolwa

Imetolewa na,
Kitengo Cha Mawasiliano Serikalini,
Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale.

Juni 29, 2024

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Nyang'hwale, S.L.P 352, Geita
Barua pepe: ded@nyanghwaledc.go.tz